**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI**

---

# MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA FEDHA WA MWAKA 2026 *[THE FINANCE BILL, 2026]*

---

Katibu wa Bunge
10 Barabara ya Morogoro
S.L.P 941
40490 Tambukareli,
**DODOMA**

24 Juni, 2026

## YALIYOMO

**1.0. UTANGULIZI** ........ **4**

**2.0. UCHAMBUZI WA MUSWADA** ........ **5**

**3.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA FEDHA WA MWAKA 2026** ........ **7**

**3.1. Sheria ambazo Kamati ilikubaliana na Mapendekezo ya Serikali** ........ 8

**3.1.1. Sheria ya Usafirishaji wa Bidhaa Nje ya Nchi, Sura ya 196** ........ 8

**3.1.2. Sheria ya Usalama Barabarani, Sura ya 168** ........ 9

**3.1.3. Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, Sura ya 161** ........ 10

**3.1.4. Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sura ya 283** ........ 11

**3.1.5. Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Sura ya 82** ........ 11

**3.1.6. Sheria ya Miamala ya Kielektroniki, Sura ya 441** ........ 12

**3.1.7. Sheria ya Ushindani, Sura ya 285** ........ 13

**3.1.8. Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290** ........ 13

**3.1.9. Sheria ya Ardhi, Sura ya 113** ........ 14

**3.1.10. Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura ya 399** ........ 15

**3.1.11. Sheria ya Madini, Sura ya 123** ........ 15

**3.1.12. Sheria ya Udhibiti wa Uingizaji wa Bidhaa Nchini, Sura ya 276** ........ 16

**3.1.13. Sheria ya Ushuru wa Stempu, Sura ya 189** ........ 17

**3.1.14. Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438** ........ 17

**3.1.15. Sheria ya Reli Sura ya 170 na Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta Sura ya 220.** ........ 18

**3.1.16. Sheria ya Rufani za Kodi, Sura ya 408** ........ 19

**3.2. Sheria ambazo zina marekebisho ya Kamati na Serikali imeridhia** ........ 20

**3.2.1. Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Sura ya 147** ........ 20

**3.2.2. Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332** ........ 24

**3.2.3. Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura ya 41** ........ 26

**3.2.4. Sheria ya Ukadiriaji Majengo katika Serikali za Mitaa Sura ya 28** 27

**3.3. Sheria ambazo Kamati imeleta jedwali la Marekebisho** ......................... 28

**3.3.1. Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura ya 197** ......................................... 28

**3.3.2. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148** .......................... 30

**3.3.3. Sheria ya Tume ya Taifa ya Mipango, Sura ya 127** ................................. 33

**4.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI** ........................................................ **34**

**4.1. Kudhibiti Magendo mipakani** ........................................................................ 34

**4.2. Kanuni za Uvuvi** ............................................................................................. 35

**4.3. Kuanzisha mifuko ya Maendeleo ya Umwagiliaji na Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo** ........................................................................................................ 36

**5. HITIMISHO** ........................................................................................................ **37**

**MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA FEDHA WA MWAKA 2026 [THE FINANCE BILL, 2026]**

---

## 1.0. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 102(1)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025 ikisomwa pamoja na kifungu cha 9(1) cha Sheria ya Bajeti Sura 439, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2026 (The Finance Bill, 2026).

**Mheshimiwa Spika,** Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2026 unakusudia kufanya marekebisho kwenye **Sheria 26**, kwa malengo yafuatayo:-

i. Kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya umeme na gesi asilia;
ii. Kuchochea uzalishaji wa bidhaa za viwanda vya ndani pamoja na kuvilinda dhidi ya ushindani usio sawa kutoka nje;
iii. Kuwezesha upatikanaji wa malighafi kwa viwanda vya ndani ya nchi na ndani ya jumuiya ya Afrika mashariki;
iv. Kupanua wigo wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali pamoja na kuimarisha mfumo wa usimamizi wa kodi;

v. Kuchochea kasi ya ulipaji wa kodi kwa hiari sambamba na kupunguza matumizi ya fedha taslimu;
vi. Kuanzisha utaratibu maalumu wa utozaji wa kodi kwa makampuni ya uchimbaji wa madini yaliyoingia mikataba na Serikali;
vii. Kuanzisha kodi ya mapato kwenye sekta ya kilimo hasa kwenye ununuzi wa mazao ya kilimo na mifugo; na
viii. Kutekeleza Mapendekezo ya Tume ya Rais ya Maboresho ya Mfumo wa Kodi.

## 2.0. UCHAMBUZI WA MUSWADA

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 100(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, Kamati ilikutana na wadau tarehe 20 na 21 Juni, 2026 ambapo ilipokea maoni yao kuhusu Muswada. Maoni hayo yaliisaidia Kamati katika uchambuzi, kuboresha na kufanya maamuzi kwa maslahi mapana ya Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** jumla ya wadau **16** walifika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao. Naomba niwatambue wadau hao kama ifuatavyo:- Tanzania Private Sector Federation (TPSF), Shirikisho la Viwanda Tanzania (CTI), Tanzania Bankers Association (TBA), Tanzania Chamber of Mines, Tanzania Fisheries Union (TAFU), Tanzania Industrial Fish Processors Association (TIFPA), Serengeti Breweries Limited (SBL), Tanzania

Breweries Limited (TBL), Tanzania Sugar Producers Association (TSPA), Tanzania Cigarette Company (TCC), Tanzania Commercial Poultry Association (TCPA), Textile and Garments Manufacturers Association of Tanzania (TEGAMAT), Chama cha Wamiliki wa Shule Tanzania (TAMONGSCO), Association of Confectionary Manufacturers, Kiwanda cha Goodwill (T) Ltd pamoja na Tanzania Grain Millers.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii inatoa mrejesho wa mashauriano kati ya Kamati na Serikali kwa Sheria 26 zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho. Sheria hizo ni:-

i. Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura ya 197;
ii. Sheria ya Miamala ya Kielektroniki, Sura ya 442;
iii. Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147;
iv. Sheria ya Usafirishaji wa Bidhaa Nje ya Nchi, Sura ya 196;
v. Sheria ya Ushindani, Sura ya 285;
vi. Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura ya 41;
vii. Sheria ya Udhibiti wa Uingizaji wa Bidhaa Nchini, Sura ya 276;
viii. Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332;
ix. Sheria ya Ukadiriaji Majengo Katika Serikali za Mitaa, Sura ya 289;
x. Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi Na. 6 ya mwaka 2025;

xi. Sheria ya Ardhi, Sura ya 113;
xii. Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290;
xiii. Sheria ya Madini, Sura ya 123;
xiv. Sheria ya Ada ya Usajili na Uhamishaji wa Magari, Sura ya 124;
xv. Sheria ya Tume ya Taifa ya Mipango, Sura ya 127;
xvi. Sheria ya Reli, Sura ya 170;
xvii. Sheria ya Tozo za Barabara na Mafuta, Sura ya 220;
xviii. Sheria ya Usalama Barabarani, Sura ya 168;
xix. Sheria ya Ushuru wa Stempu, Sura ya 189;
xx. Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 438;
xxi. Sheria ya Rufani za Kodi, Sura ya 408;
xxii. Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura ya 399;
xxiii. Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, Sura ya 161;
xxiv. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148;
xxv. Sheria ya Elimu na Mafunzo na Ufundi Stadi, Sura ya 82; na
xxvi. Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sura ya 283.

## 3.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA FEDHA WA MWAKA 2026

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya uchambuzi wa Sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho ambapo baadhi ya mapendekezo, Kamati ilikubaliana nayo na mengine haikukubaliana nayo na hivyo kuitaka Serikali kufanya

marekebisho. Maelezo ya kina kuhusu uchambuzi wa Kamati pamoja na mrejesho wa mashauriano ni kama ifuatavyo:-

## 3.1. Sheria ambazo Kamati ilikubaliana na Mapendekezo ya Serikali

### 3.1.1. Sheria ya Usafirishaji wa Bidhaa Nje ya Nchi, Sura ya 196

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inakusudia kufanya mabadiliko katika Sheria hii ili kuanza kutoza ushuru kwa mauzo nje kwa bidhaa mbalimbali kama ifuatavyo:-

i. **asilimia 30** ya thamani ya mzigo (FOB) au **shilingi 200** kwa kila kilogramu moja kutegemeana na kiwango kitakachokuwa kikubwa kwenye taka za karatasi;

ii. **asilimia 10** ya thamani ya mzigo (FOB) au **shilingi 200** kwa kila kilogramu kutegemeana na kiwango kitakachokuwa kikubwa kwenye madini ya *Quartz;*

iii. kuweka tozo ya **shilingi 50** kwa kila kilo ya pumba za ngano (wheat bran), mpunga (rice bran), mahindi (maize bran) pamoja na mashudu ya pamba (cotton cake) na alizeti (sunflower cake) zinazosafirishwa kwenda nje.

**Mheshimiwa Spika,** lengo la mapendekezo hayo ni kuchochea uongezaji wa thamani wa bidhaa hizo ndani ya nchi pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa malighafi kwa viwanda vinavyotumia bidhaa hizo kama malighafi.

### 3.1.2. Sheria ya Usalama Barabarani, Sura ya 168

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inakusudia kufanya marekebisho katika sheria hii kwa lengo la kuruhusu gari au trela lililosajiliwa kwa mujibu wa sheria ya usajili ya Tanzania Zanzibar kutumika Tanzania Bara likiwa na namba za usajili za Tanzania Zanzibar, pale ambapo tofauti ya kodi zote kwenye gari au trela husika zimelipwa kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikubaliana na pendekezo hili hata hivyo iliielekeza Serikali kuanza utekelezaji wa marekebisho ya Sheria hiyo kuanzia tarehe 01 Januari, 2027 ili kuweza kufanya maandalizi ya utekelezaji wa utaratibu wa magari yatakayokuwa yanaingia Tanzania Bara na usajili wa Tanzania Zanzibar kwa kipindi kifupi kisichozidi miezi mitatu. Baada ya majadiliano Serikali ilikubaliana na mapendekezo

ya Kamati kama yanavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho ya Serikali.

### 3.1.3. Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, Sura ya 161

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imekusudia kufanya marekebisho katika sheria hii kwa lengo la kuongeza vyanzo vya mapato vya mfuko wa kugharamia bima ya afya kwa wote. Vyanzo, vinaovyoongezwa ni kuanza kutoza kiasi cha **shilingi 20** katika kila sigara **1000** na **shilingi 10** katika kila **kilo 1** ya sukari inayozalishwa nchini au inayoagizwa nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya mashauriano baina ya Serikali na Kamati, Serikali ilikubali kutototoza **shilingi 10** kwa kila kilo ya sukari inayozalishwa nchini na badala yake kutoza **shilingi 20** katika Sukari inayoingizwa kutoka nje. Marekebisho hayo yataongeza mapato ya Serikali kwa **Shilingi bilioni 10.** Marekebisho ni kama yanavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho ya Serikali.

### 3.1.4. Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Sura ya 283

**Mheshimiwa Spika,** Sheria hii inakusudiwa kufanyiwa maboresho katika kifungu cha nane kinachohusu mgawanyo wa mapato yanayopaswa kwenda Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA) na Mfuko Mkuu wa Serikali. Lengo ni kubainisha ada za utalii wa picha katika maeneo ya wazi (fees payable for non consumptive tourism in open areas) zilizokuwa zinakusanywa na Mamlaka ya Mapato (TRA) na zilikuwa hazirejeshwi TAWA pamoja na ada ya pango (concession fees).

**Mheshimiwa Spika,** lengo la marekebisho haya ni kuwezesha mapato yanayokusanywa na TRA kutokana na upigaji picha wa kitalii na ada ya pango kurejeshwa katika vijiji husika ambavyo ardhi yao inatumika kwa ajili ya shughuli hizo ili kuviendeleza na kuchochea maendeleo ya kiuchumi.

### 3.1.5. Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Sura ya 82

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inakusudia kufanya marekebisho katika sheria hii ili kuweka bayana

wigo wa msamaha kwa taasisi za Serikali zisizopaswa kulipa Tozo ya Maendeleo ya Ufundi Stadi. Hatua hii itasaidia kuondoa changamoto katika utekelezaji wa sheria hiyo.

### 3.1.6. Sheria ya Miamala ya Kielektroniki, Sura ya 441

**Mheshimiwa Spika**, Serikali inakusudia kufanya maboresho katika Sheria hii kwa sababu kuu mbili. Moja ni kumpa mamlaka Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha kuainisha malipo yanayopaswa kufanyika kwa njia ya kielektroniki kupitia gazeti la Serikali na pili, kuweka sharti la uthibitisho wa malipo ya kidigitali kuwa rejea ya lazima itakayotumika kuidhinisha maombi ya uhamishaji wa mali kama vile ardhi, majengo na magari.

**Mheshimiwa Spika,** lengo la maboresho haya ni kupunguza matumizi ya fedha taslimu, kuzuia vitendo vya uhalifu pamoja na kurahisisha usimamizi na ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Aidha, utaratibu huu utaanza kutumika kwenye miamala inayofanyika katika biashara ya ardhi na majengo, michango na ada za shule pamoja na vyuo, manunuzi kwenye maduka makubwa (malls), malipo ya nauli, ada na tozo, kumbi za

sinema na sherehe, vituo vya kujaza mafuta, ununuzi wa magari na maeneo ya maonesho ya biashara ya kimataifa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuleta mapendekezo hayo kwani umekuwa ni ushauri wa Kamati kwa muda mrefu.

### 3.1.7. Sheria ya Ushindani, Sura ya 285

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imekusudia kurekebisha sheria hii kwa lengo la kuweka kiwango cha **asilimia 0.5** ya mapato ghafi ya Mamlaka za Udhibiti kitakachokuwa kinawasilishwa kwenye Baraza la Ushindani kila mwezi. Hatua hii ina lengo la kuondoa changamoto iliyopo hivi sasa ambapo mamlaka hizo zilikuwa zikiwasilisha mapato hayo kama hisani pamoja na kwamba utaratibu huo ulikuwa umebainishwa katika kanuni.

### 3.1.8. Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inakusudia kufanya marekebisho kwenye Sheria hii kwa malengo yafuatayo:-

i. Kuondoa jukumu la ukusanyaji wa mapato ya pango la ardhi kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania kwenda Mamlaka ya Serikali za Mitaa;
ii. Kuweka mgawanyo wa mapato ya **asilimia 20** yanayotokana na kodi ya pango la ardhi kwa mgawanyo wa **asilimia 10** kwenda Wizara ya Ardhi kwa ajili ya upimaji wa ardhi na **asilimia 10** kubaki kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa ajili ya kuwezesha ukusanyaji wa kodi hiyo;
iii. Kumpatia Mamlaka Waziri wa Fedha kutangaza viwango vitakavyotozwa kwenye matangazo pamoja na ukusanyaji wa kodi ya mabango na majengo; na
iv. Mamlaka ya Serikali za Mitaa kutenga **asilimia 15** ya mapato ghafi kwa uwiano wa **4:4:2:5** ambapo **asilimia 4** ni kwa ajili ya mikopo ya vijana, **4** kwa ajili ya mikopo ya wanawake, **2** kwa ajili watu wenye ulemavu na **5** kwa ajili ya ujenzi na maboresho ya miundombinu ya biashara.

### 3.1.9. Sheria ya Ardhi, Sura ya 113

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria hii ili kuweka

mgawanyo wa **asilimia 20** ya mapato yanayotokana na kodi ya pango la ardhi (land rent) yanayorejeshwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa ambapo **asilimia 10** kupelekwa Wizara yenye dhamana na masuala ya Ardhi na **asilimia 10** kupelekwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

### 3.1.10. Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura ya 399

**Mheshimiwa Spika**, Sheria hii inafanyiwa maboresho ili kujumuisha Sheria ya Kudhibiti Uingizaji wa Bidhaa Nchini, Sura ya 276 na Sheria ya Kodi ya Usafirishaji wa Bidhaa Nje ya Nchi, Sura ya 196 katika orodha ya sheria zinazosimamiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Aidha, marekebisho hayo pia yanalenga kuondoa Sheria ya Ukadiriaji Majengo katika Serikali za Mitaa, Sura ya 289 miongoni mwa Sheria zinazosimamiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania.

### 3.1.11. Sheria ya Madini, Sura ya 123

**Mheshimiwa Spika**, sheria hii inafanyiwa marekebisho ili kuanzisha Mfuko wa Utafiti wa Madini (mineral high resolution survey). Chanzo cha mapato ya Mfuko huo ni **asilimia 10** ya mapato yatokanayo na Sekta ya Madini. Aidha,

Fedha hizo zitaingizwa kwenye akaunti maalumu itakayofunguliwa Benki Kuu, na matumizi yake kufanyika baada ya kupata idhini ya Mlipaji Mkuu wa Serikali. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha utafiti na uwekezaji katika sekta ya madini nchini. Vilevile, Serikali imeboresha kifungu hicho kwa kufuta maneno *mineral high resolution survey* na badala yake kuweka maneno *geoscientific surveys* ili kutekeleza maoni ya Kamati kama inavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho ya Serikali. Aidha, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kuunganisha Mfuko huu na Mfuko wa Mafuta na Gesi ili kuunda Mfuko kwa ajili ya vizazi vijavyo.

### 3.1.12. Sheria ya Udhibiti wa Uingizaji wa Bidhaa Nchini, Sura ya 276

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imekusudia kufanya marekebisho katika sheria hii kwa lengo la kutekeleza makubaliano ya Itifaki ya Uanzishwaji wa Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Masharti hayo yanaelekeza nchi wanachama kuzuia ubaguzi wa kikodi ili kuruhusu

biashara huria na kuleta ushindani wa haki. Vilevile, marekebisho hayo yamekusudia kuvutia uwekezaji nchini, kuchochea mauzo nje ya nchi na kulinda uzalishaji wa ndani.

### 3.1.13. Sheria ya Ushuru wa Stempu, Sura ya 189

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inakusudia kufanya marekebisho katika sheria hii ili kuhakikisha kuna usawa wa utozaji kodi, kuongeza wigo wa kodi na kulinda thamani ya mapato ya Serikali.

### 3.1.14. Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura 438

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imekusudia kufanya marekebisho kwenye Sheria hii ili:-

i. Kuweka sharti la mtu ambaye anatakiwa kulipa kodi ya mapato yatokanayo na ajira au biashara kuomba namba ya mlipa kodi ndani ya siku **15** tangu kuanza kwa shughuli husika;
ii. Kuweka sharti kwa Kampuni inayojihusisha na ujenzi pamoja na sekta ya uziduaji kuwasilisha kumbukumbu ndani ya siku **30** kwa njia ya kielektroniki ya makampuni ambayo yamepewa zabuni (sub contracted) kwa Kamishna Mkuu kwa kutumia fomu maalumu itakayobainishwa;

iii. Kumpa Kamishna Mkuu mamlaka ya kuuza kwa njia ya mnada au kwa makubaliano binafsi kwa bidhaa zilizotaifishwa zinazoweza kuharibika haraka; na

iv. Kuweka masharti ya adhabu kwa makampuni yatakayokuwa yamejihusisha na ukwepaji wa kodi kwa njia ya kuhamisha mapato (Transfer pricing arrangements).

**Mheshimiwa Spika**, baada ya majadilinao na Serikali pamoja na mambo mengine ilikubali kuweka sharti la kuondoa misamaha ya kodi iliyotolewa chini mikataba ya msingi ya Sekta ya Madini pale ambapo itabainika muwekezaji ametumia vibaya misamaha hiyo.

**3.1.15. Sheria ya Reli Sura ya 170 na Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta Sura ya 220.**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inakusudia kufanya marekebisho katika Sheria hizi ili kuweka mgawanyo wa mapato ya Mifuko yenye vyanzo maalumu kama ifuatavyo:

i. **Asilimia 70** itawasilishwa moja kwa moja katika akaunti za mifuko husika;

ii. **Asilimia 25** itawasilishwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali; na

iii. **Asilimia 5** itawasilishwa katika akaunti maalumu iliyopo Benki Kuu kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu saidizi katika maeneo maalumu ya kiuchumi au maeneo ya uzalishaji kwa mauzo ya nje.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii kwa sababu itasaidia mifuko kuwa na rasilimali fedha endelevu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi pamoja na ulipaji wa madeni ya wakandarasi, wazabuni na watoa huduma. Hata hivyo, Kamati iliishauri Serikali badala ya **asilimia 5** ya mapato kuelekezwa kwenye maeneo huru ya mauzo nje ya nchi, ielekezwe kwenye maeneo mengine yenye lengo la kuongeza thamani. Jambo ambalo Serikali ilikubali na marekebisho ni kama yanavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho ya Serikali.

### 3.1.16. Sheria ya Rufani za Kodi, Sura ya 408

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imekusudia kufanya maboresho kwenye Sheria hii kwa lengo la kuongeza muda wa kutatua mgogoro nje ya mahakama kutoka siku **60** za sasa hadi siku **90.** Aidha, marekebisho hayo yanaweka masharti ya

Bodi ya Rufani pamoja na Baraza la Rufani ya kodi kujiridhisha kwamba wahusika wako tayari kumaliza mgogoro nje ya bodi na Baraza. Aidha, Bodi na Baraza zinaweza kuongeza muda wa kuendelea na utatuzi endapo siku 90 zimeisha na wahusika wamewasilisha maombi ya nyongeza ya muda ili kumaliza mgogoro.

## 3.2. Sheria ambazo zina marekebisho ya Kamati na Serikali imeridhia

### 3.2.1. Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Sura ya 147

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba Sheria hii inarekebishwa kwa malengo mbalimbali ikiwemo:-

i. Kubadili utaratibu uliokuwepo wa kufanya mabadiliko ya viwango vya ushuru wa bidhaa baada ya miaka mitatu na kuanzisha utaratibu mpya wa kubadilisha kila mwaka kwa kuangaliwa makisio ya mfumuko wa bei ukijumlisha na **asilimia 2**. Lengo ni kulinda thamani ya fedha na kuongeza mapato ya Serikali;

ii. Kuanzisha utaratibu wa kutoza kodi ya ushuru wa bidhaa kwa watengeneza maudhui ambao hawajasajiliwa nchini na kuyauza

nchini kwa watu ambao hawana wajibu wa kulipa wala kufanya marejesho ya kodi. Lengo ni kuweka mawanda sawa ya utozaji wa kodi hiyo;

iii. Kutoza ushuru wa bidhaa kwa **asilimia 20** kwa magari yenye miaka **8** na yasiozidi miaka **10**, **asilimia 40** kwa magari yenye miaka **10** lakini hayazidi miaka **20** na **asilimia 50** kwa magari yanayozidi miaka **20**;

iv. Kuanzisha kodi ya ushuru wa bidhaa kwa **asilimia 5** kwenye dau la kamali katika michezo ya kubahatisha ya kasino, dubu na michezo ya kidijiti;

v. Kusamehe kodi ya ushuru wa bidhaa kwenye makampuni ya madini yaliyoingia mikataba na Serikali iliyoridhiwa na Baraza la Mawaziri kwenye bidhaa zitakazoingizwa nchini ili kuwezesha utekelezaji wa miradi ya uwekezaji mkubwa katika sekta ya madini;

vi. Kufanya mabadiliko ya viwango vya ushuru wa bidhaa kwenye bidhaa zisizo za petroli kwa **asilimia 8**; na

vii. Kuanzisha kodi ya ushuru wa bidhaa wa **asilimia 20** kwa bidhaa za maua bandia,

**asilimia 10** kwenye mashine za kukaushia kucha na **asilimia 5** kwa pikipiki.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikuwa na mapendekezo tofauti katika masuala mbalimbali yanayopendekezwa kurekebishwa katika sheria hii. Baada ya mashauriano na Serikali, Kamati ilikubalina na Serikali katika maeneo yafuatayo:-

i. Kutumia mfumuko wa bei halisi wa mwaka uliotangulia na mwaka unaoendelea (year on year actual inflation rate for the period ending March);

ii. Kupunguza kiwango cha kodi ya ushuru wa bidhaa kutoka **asilimia 20** inayopendekezwa hadi **asilimia 18** kwa magari yenye umri kati ya miaka **8** hadi **10**;

iii. Kuondoa kodi ya ushuru wa bidhaa ya **asilimia 5** kwenye pikipiki za miguu miwili maarufu kama boda boda zenye ukubwa wa injini ya cc **50** hadi **250**;

iv. Kuweka ukomo wa misamaha ya ushuru wa bidhaa ikwenye sipokuwa bidhaa za petroli zinazotolewa msamaha kwenye Makampuni ya madini yenye mikataba na Serikali ili kuzuia matumizi mabaya ya

misamaha hiyo. Hivyo, ilipendekezwa misamaha hiyo itumike wakati wa kuanzisha mradi tu na itakoma pale uzalishaji utakapoanza;

v. Kuongeza kiwango cha ushuru wa bidhaa kwenye vinywaji vya kuongeza nguvu vinavyoingizwa nchini kutoka nje zinazotambuliwa kwa HS Code 2202.99.00 kwa **shilingi 100** ili kuongeza fedha kwenye Mfuko wa wa Bima ya Afya kwa wote; na

vi. Kuondoa ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha **asilimia 5** kwenye thamani ya dau la michezo ya kubahatisha na badala yake kutoza kwenye mapato ya ushindi yatokanayo na michezo hiyo kutoka **asimilia 12** ya sasa hadi **asilimia 15.**

**Mheshimiwa Spika,** mabadiliko hayo yanaonesha nia thabiti ya **Mhe**. **Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** katika kuhakikisha analinda mapato ya Serikali na kukuza uchumi. Marekebisho hayo ni kama yanavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho ya Serikali.

### 3.2.2. Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba Sheria hii inarekebishwa kwa malengo mbalimbali yakiwemo:-

i. Kumuwezesha Waziri kusamehe kodi ya mapato kwa wawekezaji mahiri waliopitishwa na Kamati ya Taifa ya Uwekezaji pamoja na wawekezaji wenye mikataba na Serikali kwenye Sekta ya Madini ambayo Serikali inahisa;

ii. Kupunguza kiwango cha kodi ya mapato kinachotozwa kwenye mapato ambayo hayajagawanywa kwa wana hisa kutoka **asilimia 30** ya sasa hadi **asilimia 15** na kusamehe kodi hiyo kwenye Taasisi za Fedha, Benki, Kampuni za Bima, Makampuni yaliyosajiliwa katika Soko la hisa la Dar es salaam na Makampuni ya madini yenye mikataba ya msingi na Serikali;

iii. Kuanzisha kodi ya mapato kwa **asilimia moja** kwenye mauzo ya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi;

iv. Kuweka bayana utaratibu wa utozaji wa kodi ya **asilimia 2** kwenye mazao ya misitu;

v. Kutambua vivutio vya kikodi vinavyotolewa kupitia Mikataba ya msingi ya Sekta ya madini ambayo Serikali imeingia na makampuni ya madini yenye leseni za uchimbaji mkubwa baada ya kuridhiwa na Baraza la Mawaziri;
vi. Kuanzisha utaratibu wa kutotoza kodi ya awali kwa wafanyabiashara wanapoanzisha biashara mpya kwa mwaka mmoja; na
vii. Kubadili viwango vya kodi kwa wafanyabishara wanaotunza na wasiotunza kumbukumbu za mauzo kutoka kiwango cha sasa cha **asilimia 3.5** hadi **asilimia 4.5** kwa mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikuwa na mapendekezo tofauti katika masuala mbalimbali yanayopendekezwa kurekebishwa katika sheria hii. Baada ya mashauriano na Serikali, Kamati ilikubalina na Serikali katika maeneo yafuatayo:-

i. Kuondoa kodi ya mapato ya **asilimia moja** kwenye mauzo ya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi;
ii. Kupunguza kiwango cha kodi kwa wafanyabiashara wasiotunza kumbukumbu wenye mapato yanayoanzia **shilingi**

**11,000,001** hadi **shilingi 200,000,000** kutoka **asilimia 4.5** hadi **asilimia 4**; na

iii. Kufuta Ibara ya 30 ya muswada iliyokuwa inapendekeza pamoja na mambo mengine kuipa mikataba ya msingi ya Sekta ya Madini nguvu dhidi ya sheria ya kodi ya mapato pale ambapo kuna kuwa na utofauti wa tafsiri.

**Mheshimiwa Spika**, haikuwa rahisi Kamati kufikia marekebisho hayo na Serikali, Kamati inampongeza Mhe. Balozi Khamis Musa Omar, Mb Waziri wa Fedha kwa uungwana wake wa kusikiliza, kutafakari na kufanyia kazi mapendekezo ya Kamati. Marekebisho hayo ni kama yanavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho ya Serikali.

### 3.2.3. Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, Sura ya 41

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ilikusudia kufanya marekebisho katika sheria hii, ili kubainisha **asilimia 10** ya mapato yanayotokana na **asilimia 5** ya kodi ya ushuru wa bidhaa kwenye dau kuwa sehemu ya mapato ya Bodi ya Michezo ya Kubahatisha. Hata hivyo, baada ya majadiliano baina ya Kamati na Serikali, Serikali iliridhia

kuondoa mapendekezo ya marekebisho hayo na badala yake ilikubali kuongeza kiwango cha kodi kinachotozwa kwenye mapato ya kodi ya ushindi (tax on winning) kutoka **asilimia 12** ya sasa hadi **asilimia 15.** Marekebisho ni kama yanavyoonekana katika jedwali la marekebisho ya Serikali.

### 3.2.4. Sheria ya Ukadiriaji Majengo katika Serikali za Mitaa Sura ya 289

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inakusudia kufanya marekebisho katika Sheria hii ili:-

i. Kuhamisha jukumu la ukusanyaji wa kodi ya majengo kutoka TRA kwenda Mamlaka ya Serikali za Mitaa; na
ii. Kubainisha utaratibu wa kukusanya mapato hayo kwa kupitia mfumo wa ununuzi wa umeme wa LUKU.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini utaratibu wa kukusanya kodi hii kupitia mfumo wa ununuzi wa LUKU unaacha nje majengo ambayo hayana umeme wa TANESCO kwenye wigo wa utozaji wa kodi hii. Hivyo, Kamati ilipendekeza Serikali kuweka utaratibu mbadala utakaowezesha ukusanyaji wa kodi hiyo kwa walio nje ya mfumo

wa LUKU. Serikali ilikubaliana na mapendekezo ya Kamati na maboresho ni kama yanavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho ya Serikali.

## 3.3. Sheria ambazo Kamati imeleta jedwali la Marekebisho

### 3.3.1. Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura ya 197

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imekusudia kupunguza kiwango cha mikopo ya muda mfupi inayochukuliwa na Serikali kutoka Benki kuu (overdraft) kutoka **asilimia 18** ya mapato halisi ya ndani ya mwaka wa fedha uliopita hadi **asilimia 14**. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha nidhamu ya matumizi ya fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kwamba Serikali imekusudia kufuta kifungu cha 69 ili kubainisha vigezo ambavyo Benki Kuu inaweza kutoa mikopo ya muda mfupi kwa Serikali endapo kutatokea matukio yasiyotabirika au yasiyozuilika.

**Mheshimiwa spika,** Kamati haikukubaliana na mapendekezo ya Serikali kwa sababu zifuatazo:

i. Mabadiliko hayo yanaondoa sharti la Benki Kuu kutokopesha Serikali na Taaaisi nyingine ya umma moja kwa moja au kwa njia nyingine;
ii. Mabadiliko hayo yanaondoa sharti la Serikali kulipa riba kwa kiwango cha soko kwa mkopo utakaochukuliwa, hivi sasa riba inayolipwa ni **asilimia 3;**
iii. Masuala yote yaliyobainishwa katika Tafsiri ya "unforeeseable or unnovoidable event" kwenye muswada hayana tofauti na Tafsiri ya maneno *Disaster* yaliyopo kwenye sheria ya Usimamizi wa Maafa. Hivyo, matumizi haya yanatakiwa kugharamiwa na Mfuko wa Dharura na si mkopo;
iv. Ibara ya 140 ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 35 hadi 39 cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439 imeanzisha Mfuko wa Dharura ambao una lengo la kumuwezesha Rais au Waziri aliyeteuliwa na Rais kwa ajili hiyo kutumia fedha zilizotengwa mahsusi kwa ajili ya shughuli fulani kulipia gharama za jambo la haraka na la dharura; na
v. Kifungu cha Tano cha Sheria ya Matumizi cha kila mwaka kinampa Waziri mwenye

dhamana ya masuala ya Fedha kukopa hadi Bajeti nzima ya Serikali kutoka ndani na nje ya nchi na malipo yake yatalipwa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, kwa sababu hizo, Kamati iliona kuwa Serikali ina mawanda mapana ya kupata mikopo kwa ajili ya kugharamia matumizi ya dharura. Hivyo basi, haikukubaliana na mapendekezo ya Serikali na imewasilisha jedwali la marekebisho ya Kamati.

### 3.3.2. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba Serikali inapendekeza kurekebisha sheria hii kwa malengo yafuatayo:-

i. Kuweka utaratibu wa kukusanya na kuwasilisha kodi ya ongezeko la thamani kwa mfumo wa zuio (withholding) ili kutambua vivutio vya kikodi vinavyotolewa kupitia Mikataba ya msingi ya Sekta ya Madini ambayo Serikali imeingia na makampuni ya madini yenye leseni za uchimbaji mkubwa baada ya kuridhiwa na Baraza la Mawaziri;

ii. Kutambua vivutio vya kikodi vinavyotolewa kupitia Mikataba ya madini ambayo Serikali imeingia na makampuni ya madini yenye leseni za uchimbaji mkubwa baada ya kuridhiwa na Baraza la Mawaziri;
iii. Kuweka utaratibu wa Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha kutangaza kwenye gazeti la Serikali vivutio vilivyowekwa kwenye Mikataba ambayo Serikali imeingia na wawekezaji katika sekta ya madini;
iv. Kuanza kutoza kodi ya ongezeko la thamani kwenye huduma za kielektroniki zinazotolewa kwa watanzania kutoka nje ya nchi kupitia masoko mbalimbali ya kidigiti;
v. Kuweka utaratibu wa kufanya marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani inayokusanywa kwa mfumo wa zuio;
vi. Kufanya maamuzi ya marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani ndani ya muda wa siku thelathini;
vii. Kutoa misamaha mbalimbali ya nyavu za kuvulia samaki, vifungashio vya maziwa, vituo vya kuchajia magari ya umeme na mita janja za kupima gesi ya petroli; na

viii. Kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye nguo zinazozalishwa ndani ya nchi na kutumika nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikubaliana na baadhi ya mapendekezo ya Serikali. Hata hivyo, iliishauri Serikali kufuta Ibara ya 98 na 99 inayopendekeza kuweka sharti kwa Kamishna wa Mamlaka ya Mapato kutoa uamuzi wa maombi ya marejesho ya kodi ya Ongezeko la Thamani ndani ya muda wa siku thelathini badala ya siku tisini. Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) hivi sasa inakabiliwa na changamoto ya kutokuwa na rasilimali watu ya kutosha pamoja na ujenzi wa baadhi ya mifumo ya TEHAMA kutokamilika. Kutokana na changamoto hiyo, pendekezo hili halitekelezeki.

**Mheshimiwa Spika**, kwa sababu hizo Kamati haikukubaliana na mapendekezo ya Serikali na imendaa jedwali la marekebisho ambalo inaamini waheshimiwa wabunge wataiunga mkono Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ya Fedha ya mwaka 2023 ilifanya marekebisho katika kifungu cha 11(1)

cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Sura 148 ili kuhairisha kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye bidhaa za mitaji zinazoingizwa kutoka nje ya nchi. Msamaha huo ulikuwa ni wa miaka **3** na unatarajia kukoma tarehe 30 Juni, 2026. Aidha, kutokana na kuwa bidhaa hizi bado hazizalishwi kwa wingi nchini na kufuatia utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayoendelea ambayo inahitaji bidhaa hizi, Kamati ilishauri Serikali kuongeza muda wa msamaha huu kwa kipindi cha miaka **3** hadi tarehe 30 Juni, 2029. Serikali ilikubali mapendekezo ya Kamati na marekebisho ni kama yanavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho ya Kamati.

### 3.3.3. Sheria ya Tume ya Taifa ya Mipango, Sura ya 127

**Mheshimiwa Spika**, Serikali inapendekeza kurekebisha Sheria hii ili kuweka utaratibu kwa miradi ya maendeleo ya Kitaifa kutathminiwa kwa kuzingatia vigezo vya kiufundi, kifedha, kimazingira na kiuchumi kabla ya kuingizwa katika bajeti ya Serikali. Lengo ni kuhakikisha kwamba miradi yote inayoingizwa kwenye bajeti ya Serikali imefanyiwa tathmini ya kina ili kupunguza gharama za utekelezaji wa miradi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikubaliana na pendekezo hili. Hata hivyo, iliishauri Serikali kuweka tafsiri ya neno "mradi wa maendeleo wa kitaifa" kwenye Sheria hiyo ili kuondoa utata unaoweza kujitokeza katika utekelezaji wa sheria hiyo. Pendekezo hili lilikubaliwa na Serikali. Aidha, katika Sheria hii Kamati pia ilishauri kuondoa kigezo cha tathmini ya kimazingira ili kutokwamisha utekelezaji wa miradi kwa kigezo hicho pale ambapo hakutakuwa na ulazima huo. Serikali ilikubali mapendekezo ya Kamati na maboresho ni kama yanavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho ya Kamati.

## 4.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati kwenye Ibara mbalimbali za Muswada, Kamati ina maoni ya ujumla yafuatayo:-

### 4.1. Kudhibiti Magendo mipakani

**Mheshimiwa Spika,** ili bajeti tuliyoipitisha itekelezwe kwa ufanisi ni lazima kudhibiti biashara za magendo. Hivi sasa biashara hizi sio tu hazilipi kodi bali baadhi ya bidhaa zinazopitia njia hii si salama kwa matumizi ya binadamu

na kuna uwezekano wa wananchi kudhurika kutokana matumizi yake. Hivyo, Kamati inaishauri serikali kutekeleza masuala yafuatayo:-

i. Vyombo vyote vya ulinzi na usalama kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato (TRA) kuhakikisha watu wote wanaofanya biashara ya magendo wanachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwa ni pamoja na kufilisiwa;
ii. Kuipa Mamlaka ya Mapato fedha za kutosha ili kuongeza rasilimali watu pamoja na vifaa vya kudhibiti magendo mipakani kwa njia ya kisasa;
iii. Kuendelea kuimarisha mifumo ya usimamizi wa mapato ya Serikali itakayowezesha kutambua na kudhibiti magendo; na
iv. Kufanya doria za mara kwa mara kwenye maeneo ambayo yameonekana kuwa sugu katika kupitisha magendo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaamini masuala hayo yakifanyiwa kazi ni wazi kwamba tutaweza kudhibiti magendo kwa kiasi kikubwa.

### 4.2. Kanuni za Uvuvi

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi wa mabadiliko mbalimbali ya viwango yanayopendekezwa na Serikali na kubaini kwamba viwango vinavyopendekezwa vya mabadiliko kwenye sekta ya

uvuvi ni vikubwa kwa wavuvi na hivyo vinaweza kusababisha Samaki wanaovuliwa nchini kuuzwa nchi jirani ili kukwepa ongezeko hilo. Hivyo Kamati inaitaka Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na uvuvi kutokufanya mabadiliko kwenye maeneo yafuatayo:-

i. Kutoongeza ada ya kila mwaka ya leseni ya vyombo vya uvuvi **hadi shilingi 400,000** na badala yake kuacha viwango vilivyopo hivi sasa;
ii. Kutoongeza ada ya kusafirisha Samaki nchini ambayo inapendekezwa kuwa **shilingi 75** kwa kilo; na
iii. Kutoongeza ushuru wakusafirisha Samaki au mazao ya uvuvi nje ya nchi kwa kati ya **shilingi 200 hadi 350** kwa kilo.

**Mheshimiwa Spika,** endapo Serikali itaendelea na viwango hivi pendekezwa ni wazi kwamba Samaki wanaovuliwa katika ziwa Victoria **watauzwa** katika masoko ya nchi Jirani kwa sababu ziwani bado kuna ugumu wa udhibiti wa mipaka.

### 4.3. Kuanzisha Mfuko ya Maendeleo ya Umwagiliaji na Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba pamoja na kwamba kuna vyanzo vingi vya mapato katika sekta ya umwagiliaji na mifugo, bado sekta hizi zinategemea kwa kiasi kikubwa bajeti ya Serikali katika kutekeleza miradi

yake. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuanzisha mifuko ya maendeleo ya Umwagiliaji na Mifugo na vyanzo vya mapato vitokane na mapato ya vyanzo vyote vilivyoko kwenye sekta hizi mbili na baadhi vitengwe na kuelekezwa kwenye mifuko husika kwa ajili ya maendeleo ya Sekta hizo.

## 5.0. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuhitimisha kwa kukushukuru wewe binafsi Mhe. Mussa Azzan Zungu, Mb Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mhe. Daniel Baran Sillo, Mb Naibu Spika kwa kuendelea kuliongoza vema Bunge lako Tukufu. Nawashukuru pia Mhe. Bal. Khamis Mussa Omar, Mb Waziri wa Fedha, Mhe. Prof. Palamagamba J.A Kabudi, (Mb) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na wenye Ulemavu), Mhe. Anthony P. Mavunde, (Mb) Waziri wa Madini, Mhe. Hamza S. Johari, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Mhandisi Mshamu Ali Munde, Mb Naibu Waziri wa Fedha na Mhe. Laurent Deogratius Luswetula, Mb Naibu Waziri wa Fedha, kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wa kuchambua Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2026.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile, napenda kumshukuru Dkt. Natu El-Maamry Mwamba, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mlipaji Mkuu wa Serikali,  Ndg. Elijah Mwandumbya na Ndg. Nsubili Akomeligwe Kajela Joshua Manaibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Ndg. Yusuph Juma Mwenda, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania. Pia niwashukuru Makamishna, Wakuu wa Taasisi na Wataalam wote kutoka Wizara ya Fedha, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Mwandishi Mkuu wa Sheria kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati katika kipindi chote cha kuchambua Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwapongeza wajumbe wa Kamati kwa umahiri, umakini na ushirikiano wao walionipatia wakati wote wa kupitia na kuchambua bajeti ya Serikali na hatimaye kukamilika kwa Taarifa hii. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo: -

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Ali Hassan Omar King, Mb | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Bal.Dkt. Pindi Hazara Chana, Mb | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Hussein Mohamed Bashe, Mb | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Innocent Lugha Bashungwa, Mb | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Esther Nicholas Matiko, Mb | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Amina Idd Mabrouk, Mb | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Stella Alex Ikupa, Mb | Mjumbe |

| | | |
|---|---|---|
| 9. | Mhe. Joseph Zacharius Kamonga, Mb | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Bahati Kenneth Ndingo, Mb | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Ally Yahya Mhata, Mb | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Kakulu Buchard Kakulu, Mb | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Dkt. Catherine Canute Joachim, Mb | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Moses Charles Bujaga, Mb | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Asma Ali Mwinyi, Mb | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Haran Nyakisa Sanga, Mb | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Devotha Daniel Mburarugaba, Mb | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Thomas Mgonto Kitima, Mb | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Enock Zadock Koola, Mb | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Nancy Hassan Nyalusi, Mb | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** mwisho lakini si kwa umuhimu, nimshukuru Ndg. Baraka Leonard, Katibu wa Bunge kwa niaba ya Watumishi wote kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu uliowezesha kufanikisha utekelezaji wa shughuli za Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Mashimba Mashauri Ndaki, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI**

24 Juni, 2026